

Huduma ya Ushauri wa Kitaalamu Kiafya ya Mkoa Mzima (SWAHILI)

Huduma inayotolewa na Kituo cha Afya ya Akili cha Queensland kwa Tamaduni mbalimbali.

Nini maana ya Huduma ya Ushauri wa Kitaalamu?

Huduma ya Ushauri wa Kitaalamu Kiafya ya Mkoa Mzima inayotolewa na Kituo cha Afya ya Akili cha Queensland kwa Tamaduni mbalimbali (Kituo) kwa watu kutoka asili isiyozungumza Kiingereza.

Huduma ya Ushauri wa Kitaalamu inatolewa kwa bure.

Ni nani anaweza kutumia huduma ya kitaalamu ya bure ?

Unaweza kuwasiliana na Kituo kama una wasiwasi kuhusu suala la afya ya akili kwa ajiri yako mwenyewe, familia au rafiki.

Huduma hii inaweza kunisaidia namna gani ?

Huduma ya Kitaalamu ya Ushauri inaweza kutoa taarifa na ushauri juu ya masuala ya afya ya akili ambayo unaweza kuwa na wasiwasi nayo, na kukuunganisha na huduma hiyo inayoweza kukusaidia

Kama misaada zaidi inahitajika, tunaweza kutoa msaada wa muda mfupi kwako katika kupata au kushughulika na huduma za afya ya akili, kwa msaada wa mfanyakazi wa afya ya akili kutoka lugha yako mwenyewe na asili yako ya kiutamaduni. The mental health worker can assist you by:

- kueleza masuala ya kitamaduni na huduma ya afya ya akili
- kusaidia kutoa mchango katika matibabu yako na mpango wa huduma
- kusaidia kutoa mchango katika matibabu yako na mpango wa huduma

- Kukutana nawe ili kujadiliana suala la afya yako ya akili katika lugha yako mwenyewe
- kukuelezea masuala yako ya afya ya akili kwa ndugu wa familia yako
- kutoa msaada wa muda mfupi, kama vile msaada au ushauri inayohusiana na tatizo la afya ya akili.

Ni msaada gani mwingine unaoweza kutolewa?

Kituo pia kina habari zilizoandikwa kuhusu ugonjwa wa akili na habari zinazohusiana katika lugha kubwa zinazojulikana.

Pia unaweza kupigia Kituo kama unataka kujadili suala lolote kuhusiana na afya yako ya akili, kama vile dalili, matibabu, dawa, na habari kuhusu huduma za afya ya akili.

Je huduma hizi ni siri?

Ndiyo, wafanyakazi wetu wa afya ya akili, kama wataalamu wengine wa afya, wamefungwa na sheria kali za Usiri na hawaruhusiwi kujadili masuala yako na watu wengine bila ruhusa yako ya moja kwa moja

Kitu gani naweza kutarajia kupokea kutaka kwa huduma ya Ushauri wa Kitaalamu?

Unaweza kutarajia kushugulikiwa kwa heshima, utu na kuzingatia faragha yako, dini na asili yako ya kiutamaduni.

Utaulizwa kutoa idhini ya maandiko kabla ya mfanyakazi wa afya ya akili wa kutoka asili ya tamaduni yako kuweza kupewa taarifa.

Jinsi ya kupigia huduma ?

Unaweza kupiga (07) 3167 8333 kama uko Brisbane au 1800 188 189 kama uko nje ya Brisbane, na omba kuongea na Mratibu wa Huduma ya Utalaamu.

Masaa yetu ya kazi ni Jumatatu hadi Ijumaa, 8.30am mpaka 5.00pm.

Siongei Kiingereza. Nitaweza kupigia huduma hii?

Unaweza kupigia huduma ya Ukalimani kwa 1314 50, kasha omba mkalimani wa lugha yako na omba kuweza kuunganishwa na Queensland Transcultural Mental Health Centre kwa (07) 3167 8333.

Mazungumzo ya pande tatu yataweza kuanza .

Naweza kuwasiliana na Kituo namna gani?

Unaweza kutembelea ofisi zetu kwenye 519 Kessels Road, MacGregor.

Unaweza kutuandikia kwa PO Box 6623, Upper Mt Gravatt, Qld, 4122.

Unaweza kutuma barua pepe tccs@health.qld.gov.au.